# TAARIFA FUPI KWA MGENI RASMI MH. GEORGE SIMBACHAWENE (MB) WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA ILIYOTOLEWA KATIKA MKUTANO WA WAGANGA WAKUU WA MIKOA NA HALMASHAURI.
# KATIKA UKUMBI WA LAPF DODOMA TAREHE 03-07 JULAI 2017

*Mh. G. Simbachawene (Mb) Waziri wa nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI*

*Mh. Ummy Mwalimu (Mb) Waziri wa Afya, M/Jamii, Jinsia, Wazee &Watoto*

*Mh. Jordan Rugimbana- Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,*

*Ndugu Katibu Mkuu, OR- TAMISEMI,*

*Ndugu Katibu Mkuu, OR –Utumishi na Utawala Bora,*

*Ndugu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango,*

*Ndugu Katibu Mkuu, Wizara ya Afya MJJW,*

*NKM- Afya, OR –TAMISEMI,*

*Ndugu Mganga Mkuu wa Serikali,*

*Ndugu Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani,*

*Ndugu Mwakilishi wa wadau wa Maendeleo,*

*Ndugu viongozi wa Wizara zetu na Taasisi zake mlioko hapa,*

*Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri,*

*Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda na Taifa*

*Waganga Wafawidhi na Wauguzi Wafawidhi wa Hospitali za Mikoa*

*Wageni waalikwa.*

*Wanahabari. Mabibi na Mabwana.*

Awali ya yote namshukuru Mungu, Kwa kutulinda na kutukutanisha tena hapa Dodoma Katika Mkutano wetu huu Muhimu wa Pili Katika Serikali yetu ya Awamu ya Tano tukiwa na Afya Njema,

**Mh. Mgeni Rasmi**, Kwa niaba ya Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, ninayo heshima kubwa, kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri wetu wote pamoja na Watendaji wote wa Wizara zetu chini ya Uongozi wa Mh. Dr John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuwatumikia Watanzania hususani katika kuboresha huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe nchini.

Tunaipongeza Wizara yetu ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Idara yetu ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe –OR TAMISEMI kwa jinsi ilivyozamilia kuleta mabadiliko ya dhati kiutendaji na utekelezaji wa Sera, Miongozo ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe nchini.

Kwa dhati kabisa tunaungana na watanzania wote Kumpongeza Rais wetu Mh. Dr John Pombe Joseph Magufuli kwa Uzalendo, Ubunifu na nia ya dhati aliyonayo ya kutuunganisha watanzania katika kulinda rasilimali za Taifa letu na mipango mikubwa ya Serikali yetu ya Kuimarisha na kuboresha Huduma za Afya nchini zitakazoendana na Tanzania mpya ya Viwanda na Uchumi wa kati.

Tunakushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuwa Mgeni rasmi katika Mkutano wetu huu wa leo, unaojumuisha Wakurugenzi wa Hospitali zetu za kanda na Taifa, Waganga na Wauguzi wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Wauguzi Wakuu wa Mikoa, Viongozi wetu wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara zetu.

Baada ya maneno haya mafupi naomba sasa niwasilishe taarifa fupi sana kutoka kwa Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri.

***Utangulizi***

**Mh. Mgeni Rasmi,** Afya ni Mtaji, Afya ni Mali, Afya ni Furaha, Afya ni Maendeleo na Afya ni Kichocheo cha ukuaji wa uchumi katika nchi yeyote duniani (Health is catalysit of any country's economic growth)

Kila Mtanzania popote alipo, Kila binadamu anayo haki ya kupata huduma bora za afya hivyo kila mmoja anao wajibu wa kulinda afya yake.

**Mh. Mgeni rasmi,** Kwanza tunapenda tuanze kuanisha mafanikio kadhaa ambayo kwa kipindi kifupi cha serikali yetu ya awamu ya tano yanatia moyo kuelekea kuwa na taifa lenye afya bora:

- Serikali kuendelea kutenga kiasi kikubwa cha fedha Bil 250 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba nchini,
- Ununuzi wa ambulances 50 kwa mikoa ya BRN,
- Serikali kudhibiti uuzaji, na unywaji na pombe inayofungashwa katika viroba,
- Uanzishaji wa mfumo mmoja wa kielectronic wa GoT HoMIS wa ukusanyaji wa taarifa na udhibiti wa mapato kwenye vituo vya huduma vilivyo chini ya Mikoa na Halmashauri. Tayari asilimia 6 ya Hospitali za umma zikiwemo hospitali zote za Mikoa zimefunga mfumo huu.
- Kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya madawa ya kulevya kwani vijana walio wengi waliathirika sana kiafya na kiuchumi na kuleta mzigo mkubwa kwa watumishi wetu walio wachache katika kuwahudumia maana tulifikia hatua mbaya sana,

- Kufanikisha upatikanaji wa fedha kugharimia ujenzi na upanuzi wa vituo vya afya 145 nchini ili viweze kutoa huduma za dharura kwa wajawazito za upasuaji
- Uamuzi thabiti wa kuanza kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya huduma na kuamua kwa dhati utekelezaji wa kuwa na mipango ya vituo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kila kituo kinakuwa na akaunti yake,
- Kutoa kibali cha kuajiri wahasibu wasaidizi 535 kwa ajili ya vituo vya afya nchini,
- Kuendelea kupanua wigo wa mpango wa malipo kwa ufanisi (RBF) kutoka Halmashauri moja hadi kufikia mikoa 8,
- kutoa ajira kwa madakitari 258 waliokuwa wameomba kwenda kufanya kazi nchini Kenya na
- Uamuzi kwa dhati wa uhakiki wa watumishi wa umma wenye sifa katika ajira na mengine mengi.

***Watumishi wa afya***

**Mh. Mgeni rasmi**, Utoaji wa Huduma bora za afya unahitaji rasilimali muhimu zifuatazo: Watoa huduma wanaojitosheleza wenye ujuzi, Vifaa tiba/dawa na Vitendanishi, Majengo bora yenye miundombinu muhimu ya maji na umeme, na fedha. Ili raslimali hizi zitumike ipasavyo ni lazima kuwepo kwa Utawala bora, mfumo thabiti wa utoaji taarifa na utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Kwa ujumla Mikoa na Halmashauri zetu zinakabiriwa na upungufu mkubwa wa watumishi hususani katika zahanati na vituo vya afya. Upungufu huu unafikia asilimia **49.5** Upungufu huu umeongezeka baada ya watumishi takiribani **3,439** kukumbwa na sakata la vyeti feki. Jumla ya zahanati **285** hazina mtumishi mwenye ujuzi hata mmoja hivyo zinaongozwa na wahudumu wa afya. Vituo vya huduma **1505** havina waganga CO au CA na vinaongozwa na wauguzi ambao kimsingi kazi yao ni uuguzi. Kwa hesabu za kawaida takribani vituo vya huduma **1790** havina tabibu hivyo ubora wa huduma za kitabibu na kiuguzi kuwa katika mashaka. Tunawashukuru sana watumishi wachache waliopo ambao wanajituma katika kuwatumikia wananchi.

**Mh. Mgeni Rasmi,** tunaomba kibali cha dharura cha kuajili watumishi **7,304** ambao kimsingi ndio nguzo kubwa katika uboreshaji wa afya ya msingi na hii itawafanya wananchi waliowengi ambao wako vijijini wafaidi ubora wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Uhitaji huu ni muhimu ukizingatia Serikali inaanza kupeleka fedha moja kwa moja kwenye vituo vya huduma na ***dhana nzima ya ugatuaji madaraka kwa umma ikiwa ni nguzo muhimu ya uboreshaji huduma za afya kwa wananchi kuelekea Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati kama kauli mbiu ya mkutano wetu***.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Tunakuhakikishia kuendelea kusimamia nidhamu na kuwajengea uwezo watumishi waliochini yetu ili watoe huduma stahiki na kukidhi matakwa ya kitaaluma.

***Miundombinu ya afya***

**Mh Mgeni Rasmi,** Ni dhahiri kuwa kila mtanzania anastahili kupata huduma za afya ya msingi karibu na eneo analoishi.

Kwa Mujibu wa MMAM mwaka 2005 Tanzania ilikuwa na vijiji vipatavyo 10,342 hivi sasa nchi yetu ina vijiji 12,545 hii ni ongezeko la takribani vijiji 2,200 na Kata zilikuwa 2,555 hivi sasa tuna kata 4420 ongezeko la takribani kata 1900, kwa upande wa Hospitali za Halmashauri/wilaya mwaka 2005 zilikuwa wilaya 114 na sasa tuna Halmashauri 184 na wilaya 139. Ni dhahiri kuwa ongezeko la vijiji na kata na ongezeko la watu hatutafikia lengo kwa asilimia 100 kama hatutakuwa na mkakati madhubuti.

Ilani yetu ya chama Tawala, na Sera ya Afya zote zinatutaka kusogeza huduma karibu na wananchi. Kwa dhati kabisa jukumu la ujenzi wa zahanati na vituo vya Afya ni letu sote kwa kushirikiana na wananchi.

Katika kutekeleza ilani na sera yetu ya kusogeza huduma hizi za afya kwa wananchi tunashauri Halmashauri kujenga kwa ukamilifu angalau zahanati 2 tu kwa kila mwaka (Jengo la OPD na RCH na nyumba angalu 3 za watumishi (two in one) pamoja na vichomea taka katika vijiji/maeneo ambayo ni kipaumbele. Kwa kufanya hivyo katika kipindi cha miaka 5 tunaweza kuongeza zahanati takribani 1,582 zenye ubora unaokubalika katika Halmashauri za wilaya na kwa upande wa vituo vya Afya angalau 2 tu kwa kila Halmashauri ya wilaya, Mji, Manispaa na jiji hivyo katika kipindi cha miaka 5 ambapo tutaweza kuongeza vituo vya afya 368 hivyo katika miaka 5 ya

utekelezaji wa Ilani ya chama tawala na mpango wetu wa MMAM tutakuwa tumeongeza vituo vya huduma 1950 hadi 2000. Utekelezaji huu unaweza ukafanyika kama jinsi ambavyo serikali iliekeza kwa Halmashauri katika ujenzi wa vyumba vya madarasa na maabara.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Katika ngazi za MSM yapo maboma 1,580 ambayo hayajakamilika yanayojumuisha majengo ya vituo na nyumba za watumishi. Tunaomba maboma haya yapatiwe fedha ili yakamilishwe,

Aidha majengo yaliyopo, mengi ya vituo vyetu ni madogo na yamechakaa hivyo kuhitaji ukarabati. Mpango wa JRF/MMAM ulisaidia sana katika kuboresha miundombinu, kutokana na mabadiliko ya viwango vya ubora wa utoaji huduma uliotolewa na Wizara yetu ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, wazee na watoto wa mwaka 2015 (Basic standard for health Facilities) ni dhahiri miundombinu ya vituo vyetu vilivyo vingi inahitaji kufanyiwa Ukarabati.

Ili kufikia ubora kwa mujibu wa miongozo na kuendana na ongezeko la watu ni bora iwe ni lazima kwa jamii kujenga shule na zahanati kama sharti la kusajiliwa kuwa kijiji. Tunaomba kuwepo na Mfuko maalumu wa uboreshaji Miundombinu ya Afya (Health Facility Infrastructure fund) kama ilivyo kwenye miundombinu ya Barabara.

***Upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.***

**Mh. Mgeni Rasmi:**

Wagonjwa wetu wanahitaji vipimo, vifaa tiba na dawa kwa ajili ya kutibu maradhi na kukidhi mahitaji yao ya kifya wanapofika vituoni. Hivyo upatikanaji wa uhakika wa rasilimali hii ni muhimu sana.

Kwa heshima tunaipongeza Serikali yetu kwa kuendelea Kutenga bajeti kubwa ya dawa na kupeleka fedha hizi kwenye akaunti za vituo vyetu zilizoko MSD. Tunakiri kuwa akaunti za vituo hivi sasa zina fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, aidha tunashukuru kwa kuendelea kulipa deni ambalo vituo vyetu vilikuwa vinadaiwa na MSD ambapo deni hilo limepungua kutoka 28 Bil hadi 19 Bil katika kipindi kifupi, hii ni ishara njema kwani upatikanji wa dawa Muhimu (Tracer Medicine) katika vituo vya huduma katika MSM umeimarika hadi kufikia asilimi 83% katika kipindi cha Jan-May 2017.

Pamoja na mafanikio haya makubwa changamoto bado ni upatikanaji wa dawa katika bohari yetu ya Dawa MSD kwani bado mahitaji ya vituo (Order fulfillment rate) yanapatikana kwa asilimia 30-40% tu ya kinachoagizwa hii inavifanya vituo viendelee kutoa huduma ya dawa isiyokidhi mahitaji yote ya wananchi wetu.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Mikoa ya Morogoro, Shinyanga na Dodoma inanunua dawa moja kwa moja kwa washitiri, pindi dawa hizo zinapokosekana MSD tofauti na Mikoa mingine ambayo haina washitiri wa aina hii, badala yake MSD ilianisha Washitiri wake wa kuuza dawa katika kila kanda ambapo kila mshitiri ameanishiwa dawa kadhaa 3 au zaidi kuuza. Tunaomba Mfumo huu wa Washitiri

katika mikoa mingine Uchambuliwe upya na Majukumu yao yaangaliwe upya kwani haujatusaidia kutatua changamoto zinazotukabili kama tulivyotarajia. Aidha tungeshauri MSD izaliwe upya tuwape fedha watununulie dawa ili kuondoa sintofahamu zinazojitokeza katika manunuzi kwani fedha ziyo tatizo hivi sasa.

**Mh. Mgeni Rasmi**, Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa ikiagiza dawa kutoka nje ya nchi, hata kwa bidhaa ambazo mali ghafi yake inapatikana hapa nchini, tunaomba msukumo wa ujenzi wa viwanda uelekezwe kwa bidhaa za afya mfano gauze, cotton wool, mashuka, drip, ORS n.k kwani Tanzania tunazo mali ghafi muhimu kama pamba, chuma n.k.

***Ugharamikiaji huduma za afya***

**Mh Mgeni Rasmi,** Ugharimikiaji wa huduma za afya ni nyenzo muhimu sana katika utoaji wa huduma bora za afya zenye usawa kwa wote, ni dhahiri kuwa kila binadamu anastahili kupatiwa huduma bora za msingi za afya wakati anaugua bila kujali kipato au uwezo wake.

Ili kufikia malengo ya usawa wa kila Mtanzania kupata unafuu wakati wa kupata huduma za afya bila kuumia (catastrophic health expenditure), ni lazima tuwe na mfumo thabiti wa kuwa na bima kwa kila mwananchi ***"Universal Health Insurance coverage"***

Utafiti wa mwaka 2015/16 (TDHIS-MIS) umeonesha kuwa kila kaya kwa mwaka hutumia Tzs 48,332 kwa ajili ya masuala ya afya (The total annual health-related expenditure per household) Hivi sasa watanzania walio na bima ya afya ni asilimia 30% (NHIF 7%, CHF

22% na Bima Binafsi na nyinginezo 1%). Kutokana na hali hiyo, wananchi wengi sana takiribani asilimia 49-60% ya wanaofika kwenye vituo vyetu wanatibiwa bila malipo (Kwa msamaha) hivyo kupelekea vituo kuwa na mzigo mkubwa wa huduma zinazotolewa bila kuchangiwa. Ili kufanikisha utekelezaji wa bima ya afya kwa wote tunashauri yafuatayo;

- Kwanza mswada wa sheria ya kila mtanzania kuwa na bima uandaliwe kwa umakini na kuwasilishwa bungeni.
- Shughuli za uhamasishaji, usajili wa wanachama na usimamizi wa mfuko wa afya ya jamii (Community Health fund) zihamishiwe na zifanywe moja kwa moja na mfuko wa afya ya Jamii chini ya usimamizi wa Halmashauri ili mfuko uwe kama mnunuzi wa huduma na vituo kuwa mtoa huduma kama ilivyo ada ya kutenganisha majukumu katika bima. Ili kuongeza wigo wa kuwawezesha wananchi kupata huduma za mfuko wa Afya ya Jamii mahali popote ndani ya Mkoa husika.
- Kwa mantiki hiyo tunashauri kila Halmashauri iwe na ofisi maalumu ya Mfuko wa Afya ya Jamii utakaoratibiwa na Mkoa na kazi yake iwe kuhamasisha, kusajiri na kutoa vitambulisho vya kielectronic kwa wanachama vitakavyokuwa vinalipiwa kila ada ya uanachama inapoisha.

Aidha ili kuhakikisha fedha zinazoelekezwa kwa masuala ya afya zinatumika ilivyokusudiwa tunaomba fedha za Oc za Halmashauri zipelekwe moja kwa moja kwenye account ya Afya ya Halmashauri badala ya kwenda kwenye pool.

### *Uimarishaji wa Hospitali za Mikoa na Kanda*

**Mh. Mgeni Rasmi**, Mfumo wa Rufaa ni Muhimu sana katika utoaji wa huduma za afya nchini, na Kila mwananchi anatarajia kupata huduma yenye ujuzi na ubora zaidi anapopatiwa rufaa kwenda kituo cha huduma cha Juu zaidi.

Tunashukuru kuzipandishwa hadhi kwa hospitali za Mikoa kuwa hospitali za rufaa za Mikoa, lengo ikiwa ni kuziimarisha ili zitoe huduma zote muhimu za kibingwa katika ngazi ya mikoa na zile za kanda katika ngazi ya Kanda. Hivi sasa tunazo Hospitali za Rufaa za Mikoa na Ngazi ya Mkoa zipatazo 27. Hata hivyo hospitali hizi Kwa ujumla Miundombinu yake na hadhi inayotakiwa kwa Hospitali za Mikoa haikidhi mahitaji ya utoaji huduma.

Tunaendelea kuomba katika bajeti zijazo kupatiwa tena fedha maalum ya kuziimarisha na kuboresha miundombinu yake hii ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi na kama CT scan na MRI awamu kwa awamu ili kuondoa kero ya wagonjwa kwenda Dar es salaam na hospitali chache za kanda kupata huduma hizi kwa gharama kubwa pia ni kivutio kikubwa kwa wataalamu hususani mabingwa kupenda kufanya mikoani na kupractice Professionalism yao katika Mikoa.

### *Afya ya uzazi na mtoto na utoaji wa huduma*

**Mh. Mgeni Rasmi,** Huduma za afya ya Uzazi na Mtoto, ndio huduma muhimu sana zinazogusa wananchi wetu walio wengi katika ngazi ya vituo vya afya ya Msingi, matokeo ya utafiti ya viashiria vya afya, na Malaria mwaka 2015/16 (TDHIS-MIS) umeonesha kuwa vifo

vitokanavyo na uzazi kutopungua kama tulivyotarajia na kupanda kutoka vifo 454 mwaka 2004/05 hadi vifo 556 mwaka 2015/16 kati ya vizazi hai 100,000. Aidha vifo vya watoto vimeendelea kupungua kutoka vifo 112 mwaka 2004/05 hadi vifo 67 kati ya vizazi hai 1000 pamoja na mafanikio haya vifo vya watoto wachanga bado ni tatizo.

Tumedhamiria kuhakikisha kuwa vifo hivi vinapungua na malengo tunayafikia kwa kujituma zaidi, kufanya usimamizi na ufuatiliaji wa karibu kwa watoa huduma wachache waliopo, pamoja na kushirikisha jamii na sekta nyinginezo hii ikiwa ni pamoja na kushughulikia matatizo ya lishe. Tunaomba ujenzi na ukarabati miundombinu ya vituo vya afya 145, pamoja na mafunzo ya utoaji dawa za usingizi kwa watoa huduma wetu ufanyike pia mpango wa kuajiri watoa huduma zaidi uharakishwe.

***Utawala Bora.***

**Mh. Mgeni Rasmi,** Utawala bora ni nguzo muhimu inayoleta matokeo chanya kwenye sekta yeyote ile ikiwemo Afya.

Wadau wa maendeleo wana mchango mkubwa sana katika kuboresha huduma za afya, Wadau wapo wengi na kuna fedha nyingi zinazotumwa kwa Serikali yetu kupitia wadau wetu wa ndani na wa kimataifa.

Tunatambua upo mwongozo wa JAST (Joint Aids Strategy Tanzania) ulioandaliwa na Wizara ya fedha miaka ya nyuma ambao haujafafanuliwa kwa watendaji ngazi za Wizara, Mikoa na Halmashauri. Aidha tunaomba kuwepo na mwongozo maalumu utakaotuongoza namna bora ya kufanya kazi na wadau. Hii itasaidia

kuwa na uelewa wa pamoja na wadau wetu wa kweli wenye nia njema, na kuwadhibiti wadau wenye malengo yao binafsi ili kudhibiti utumiaji wa rasilimali muhimu zinazoendeana na vipaumbele vya Serikali.

**Mh. Mgeni Rasmi,** Kuwepo kwa miongozo thabiti ni muhimu katika kutekeleza shughuli zetu, tunatambua kuwa ipo miongozo na maelekezo kadhaa ambayo inahitaji kupitiwa upya hii ni pamoja na mwongozo wa Uchangiaji huduma (Costsharing) wa Mwaka 1997 tunatambua changamoto iliyojitokeza kuhusu mwongozo huu. Hivyo tunashauri maelekezo muhimu ya matumizi ya fedha hizi yatolewe badala ya kila mmoja kufanya anavyoona inafaa ukizingatia hizi ni fedha na tayari baadhi ya mikoa ina hoja za ukaguzi. Mfano Mwongozo hauruhusu fedha za uchangiaji kulipa on call allowance, kufanya ukarabati wa zaidi ya Tshs 500,000 bila kibali cha Katibu Mkuu Afya na wakati huo huo Hospitali hizi hivi sasa zipo chini ya OR-TAMISEMI kiutawala, hatuna haja ya kukwepana na CAG wakati mwongozo unaweza ukatolewa na kutupa uhuru wa kuamua kwa manufaa ya Hospitali na Watumishi na Wananchi wetu.

**Mh. Mgeni Rasmi**, Mipango Kabambe ya afya ya Halmashauri CCHP na Mipango ya vituo ni Muhimu sana katika maboresho ya sekta ya afya. Pamoja na hatua kubwa tuliyofikia uandaaji wa mipango ya Vituo imeendelea kuwa na changamoto kadhaa hii ni pamoja na kutumia muda mrefu kukamilisha mipango hii (miezi 7-8), ukichangiwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya Plan Rep tool, na uwezo wa kamati za usimamizi wa vituo katika uandaaji wa Mipango.

Tunaomba mwongozo wa CCHP upitiwe upya ili kuendana na mabadiliko haya ya DHFF, Version ya Plan Rep ifanyiwe kazi mapema kuepuka mabadiliko ya kila mara na Halmashauri na Mikoa zijengewe uwezo tena ukizingatia kuwa kuna mabadiliko makubwa ya kiuongozi katika ngazi hizi.

***Mfumo wa utoaji wa Taarifa za afya.***

**Mh, Mgeni Rasmi,** Mwisho naomba niongelee suala la mfumo wa utoaji taarifa katika sekta ya Afya.

Takwimu bora ni nguzo muhimu ya maamuzi na uandaaji wa mipango bora. Katika eneo hili tumeanza kupiga hatua ukilinganishwa na miaka ya nyuma, mfumo wa GoT HOMIS, DHIS2 eLMIS, MTUHA n.k. pamoja na mifumo hii bado kuna changamoto kubwa ya takwimu ukizingatia uhaba wa watumishi wa afya na wataalamu wa takwimu kwenye vituo vyetu. Tunashauri kuwe na Mfumo mmoja tu unaosomana wa ukusanyaji wa takwimu katika ngazi za vituo vya utoaji huduma kwani ngazi hizi zinatofautiana (Ngazi ya Afya ya Msingi, Mkoa, Kanda, na zile za ngazi ya Taifa). Hii ni kutokana na utofauti wa ngazi hizi

***Kinga dhidi ya Magonjwa.***

**Mh. Mgeni Rasmi,** Kinga ni bora kuliko tiba. Tunapongeza kwa dhati namna ambavyo Mh. Rais alivyoelekeza na utekelezaji wake ulivyofanyika kwa haraka kwa Halmashauri kwenda kuchukua dawa za kuua viluwiluwi vya mbu wa malaria, pia tunawapongeza Mawazziri wetu kwa jinsi mnavyoshirikiana kusaidia mapambano dhidi ya maradhi kama TB, Magonjwa yasiyokuwa ya Kuambukiza

n.k. Tunaomba viongozi wetu muendelee na msukumo huu, hii ikiwa ni pamoja na Kila kaya kuwa na choo

Utafiti uliofanyika mwaka 2015/16 kupitia TDHIS –MIS ulionesha ni asilimia 19 tu ya kaya ndizo zina vyoo bora na asilimia 65 ya kaya hazina vyoo bora. Kwa maeneo ya vijijini asilimia 86 hazina vyoo bora na asilimia 10 ya kaya zote nchini hazina vyoo kabisa.

Mh. Mgeni rasmi, lipo tatizo kubwa la miundombinu ya maji taka katika miji yetu mikubwa hii ni sambamba na utengaji wa maeneo ya dampo na machinjio. Mvua zinapozidi kidogo imekuwa ni tishio kubwa na milipuko ya ugonjwa wa kipindupindu, mfano hivi sasa tangu ugonjwa huu wa kipindupindu utokee mwezi August 2015 zaidi ya watanzania 25,528 na vifo 401 na mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro ndio imekuwa na wagonjwa wengi zaidi.

Tunaomba changamoto hizi za vyoo bora, miundombinu ya maji taka na maji safi na mapambano dhidi ya magonjwa ya milipuko, sekta nyingine kama ya miundombinu, ardhi, mipango miji na maji ziwajibike ipasavyo kwani mchango wao ni mkubwa katika udhibiti wa milipuko.

**Mh. Mgeni Rasmi:** Kwa mara nyingine tena tunatoa shukrani zetu za dhati kwako kwa kutenga muda wako kukutana nasi, aidha, tunapenda kuahidi kwa dhati kabisa kuwa tuko imara katika kulitumikia taifa letu na tutaendelea kuwa wabunifu kukabiliana na changamoto na kwenda na kasi ya serikali ya awamu ya tano na TAMISEMI Mpya.

*Imewasilishwa na**:  Dr. Leonard Subi- M/kiti wa RMO**-Tanzania Bara.*

**Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania.**